

# Hekima ya Mungu

Adrian Ebens

# Hekima ya Mungu

*Utangulizi kwa Utata Mkuu*

Adrian Ebens

Kimechapishwa na

MARANATHA MEDIA

fatheroflove.info

Kimeandikwa kwa muundo wa makala, Marchi 2010.
Kilichapishwa Februari, 2016
kiliboreshwa Aprili 2018

# Yaliyomo

1. Baba Yetu ........ 4

2. Mfalme wa Vyote ........ 7

3. Hekima Ya Mungu ........ 10

4. Usawa ........ 14

5. Mapenzi ........ 17

6. Mgogoro Unazuka ........ 18

7. Aliumba kwa Mfano Wake ........ 22

8. Baba wa Uongo ........ 27

9. Wanadamu Kudanganywa ........ 29

10. Muhtasari ........ 33

12. Msingi wa Babeli ........ 36

13 Kiini cha Babeli ........ 40

14. Mstari wa Ukoo ........ 44

15. Wito wa Kutoka Babeli ........ 48

# 1. Baba Yetu

Yesu aliposogewa na wanafunzi wake wakati mmoja, walimwomba ombi muhimu sana:

> **Luka 11:1** Siku moja, Yesu alikuwa mahali fulani akiomba. Alipomaliza kuomba, mmoja wa wanafunzi Wake akamwambia, "Bwana, tufundishe kuomba, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake."

Jibu ambalo Yesu alitoa linatwambia jambo la msingi kabisa ambalo tunahitaji kujua kumhusu Mungu. Tendo la ombi ni kutafuta kuzungumza na kuwasiliana na Mungu. Neno ambalo Yesu alitumia kama hoja yake ya kwanza ya kurejerea linazungumza kwa utambulisho wa msingi wa Mungu na yeye ni nani. Hivi ndivyo Yesu alitwambia kumtamkia Mungu tunapoomba.

> **Luka 11:2** Akawaambia, "Mnapoomba, semeni hivi: "'Baba yetu uliye mbinguni, Jina Lako litukuzwe, Ufalme Wako uje

Baba yetu. Kando na chochote kile ambacho tunaweza zingatia, mwanzo kabisa Mungu ni Baba yetu. Maelezo haya rahisi yanatwambia mengi kumhusu Mungu. Yanatwambia kwamba zaidi ya yote Mungu ni kiumbe wamahusiano. Anataka tumtamkie kwa majina ya uhusiano. Jina Baba halizungumzii uwezo na nguvu tu, bali pia linazungumzia jinsi ya uhusiano wake na muunganisho na ulimwengu. Yeye ni Baba, au chanzo, cha vitu vyote. Hivyo basi Mungu ni Baba wa namna gani?

Wakati mmoja Musa alimuomba Mungu amdhihirishie utukufu wake, au kile ambacho kilikuwa cha kipekee kumhusu Mungu. Hivi ndivyo Mungu alijibu:

> **Kutoka 34:5,6** Bwana akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la Bwana. Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli.

Zingatia kile Mungu alimuonyesha Musa. Alizungumza juu ya tabia yake. Hili ndilo jambo tukufu zaidi kuhusu Mungu – tabia yake. Yeye ni mwenye huruma, neema, utulivu, mwingi wa wema na ukweli. Katika ulimwengu

tunaoishi ndani yake, tabia hizi ni nadra sana, lakini tunapozishuhudia kwa wengine, wengi wetu wanashukuru kwa kina. Mtume Yohana alitupa jumla ya tabia ya Mungu aliposema:

> **1 Yohana 4:8** Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo.

Mungu ni Baba mwenye upendo ambaye anajali kwa ndani kuhusu viumbe vyake vyote. Hivyo uumbaji wake ni mkubwa kiasi gani? Bibilia inatwambia kuwa ni Baba wa mbingu yote na dunia.

> **Efe 3:14,15** Kwa sababu hii nampigia Baba magoti, ambaye kwa Yeye ubaba wote wa kila jamaa za mbinguni na za duniani unaitwa.

Ulimwengu wote ni miliki ya Baba yetu aliye mbinguni, na kila mtu katika ulimwengu huu ni sehemu ya familia yake. Kwa vile kuna watu wengi, tunaweza jaribiwa kudhani kuwa Mungu hafikirii kuhusu kila mtu na wengine wanaweza sahaulika, lakini sikiza kwa makini kile Yesu alisema kuhusu hili.

> **Luka 12:6,7** Mnajua kwamba shomoro watano huuzwa kwa senti mbili? Lakini Mungu hamsahau hata mmoja wao. Naam, hata idadi ya nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa. Kwa hiyo msiogope, ninyi ni wa thamani kuliko mashomoro wengi.

Mungu hamsahau yeyote. Anajua kila kitu kutuhusu. Na ana nia ya ndani kwa maisha yetu na kile tunachofanya na kile tunachowaza. Kwa kweli hawachi kutuwazia.

> **Zaburi 40:5** Ee Bwana, Mungu wangu, umefanya kwa wingi Miujiza yako na mawazo yako kwetu; Hakuna awezaye kufananishwa nawe; Kama ningependa kuyatangaza na kuyahubiri, Ni mengi sana hayahesabiki.

Ana mipango ya kipekee kwetu na anaota juu ya kile tunachoweza kuwa.

> **Yer 29:11** Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.

Kila kitu chema tulichonacho kinatoka kwake.

> **Yakobo 1:17** Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kutoka kwa Baba wa mianga, ambaye Kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.

Onyesho la ajabu kabisa la jinsi Mungu anavyohisi kutuhusu ni kile alichokisema wakati wa Ubatizo wa Mwanawe wa Kipekee – Yesu. Hiki ndicho alichokisema:

> **Mathayo 3:17** Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye.''

Mungu alimpenda Mwanawe kama mwanadamu. Alipendezwa sana naye. Sehemu kuu kuhusu hili ni kuwa katika kutambua kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, tunaweza shuhudia kukubalika sawa na huku.

> **Efe 1:6** Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa.

Tutachunguza zaidi kuhusu jukumu la Yesu na mbona akaja duniani na mbona tunaweza na kuhitaji kukubalika kupitia kwake. Lakini hoja ya msingi ambayo tunahitaji kutilia mkazo hapa ni kuwa Mungu ni Baba mwenye upendo na tefu ambaye anatujali kwa kina na anatuwaza katika kila kipengele cha maisha yetu.

## 2. Mfalme wa Vyote

Katika sura iliyopita tuligundua kwamba Mungu ni Baba mwenye upendo ambaye anawaza kutuhusu daima na anamipango na ndoto za maisha yetu ya baadaye. Pia tuligundua kuwa ni Baba wa ulimwengu wote. Katika sehemu hii, tunataka kuangalia ni sifa zipi zinazomruhusu Mungu kuwa katika nafasi hii na kufanya mambo anayoyafanya.

Jambo la kwanza ambalo Bibilia inatwambia ni kwamba Mungu ni Bwana na Mfalme wa kila kitu.

> **1 Kor 8:6** Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka...

> **1 Tim 1:17** Basi, Mfalme wa milele, asiye na mwisho, asiyeonekana, aliye Mungu pekee, apewe heshima na utukufu milele na milele. Amen.

> **Kum 6:4** Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.

Baba ni Mungu mmoja ambaye kwake vitu vyote vinatoka. Mungu hajapokea nguvu zake, hekima au maarifa kutoka kwa mtu yeyote mwingine. Kila kitu tuonacho kinatoka kwake.

> **Isa 40:10-15** Tazameni, Bwana Mungu atakuja kama shujaa, Na mkono wake ndio utakaomtawalia; Tazameni, thawabu yake i pamoja naye, Na ijara yake i mbele zake. Atalilisha kundi lake kama mchungaji, Atawakusanya wana-kondoo mikononi mwake; Na kuwachukua kifuani mwake, Nao wanyonyeshao atawaongoza polepole. Ni nani aliyeyapima maji kwa konzi ya mkono wake, na kuzikadiri mbingu kwa shubiri, na kuyashika mavumbi ya dunia katika pishi, na kuipima milima kwa uzani, na vilima kama kwa mizani? Ni nani aliyemwongoza roho ya Bwana, na kumfundisha kwa kuwa mshauri wake? Alifanya shauri na nani, ni nani aliyemwelimisha na kumfunza njia ya hukumu, na kumfunza maarifa, na kumwonyesha njia ya fahamu? Tazama, mataifa ni kama tone la maji katika ndoo, huhesabiwa kuwa kama mavumbi membamba katika mizani; tazama, yeye huvinyanyua visiwa kama ni kitu kidogo sana.

> **Zaburi 36:7-9** Ee Mungu, jinsi zilivyo na thamani fadhili zako! Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa zako. Watashibishwa kwa unono wa nyumba yako, Nawe utawanywesha mto wa furaha zako. Maana kwako Wewe iko chemchemi ya uzima, Katika nuru yako tutaona nuru.

Mungu yuko kila mahali, kumaanisha nguvu zake hazina kikomo; hakuna mwisho wake. Nguvu zinazopatikana katika matrilioni na matrilioni ya chembe zinatoka kwake. Nguvu hiyo ni zaidi ya ufahamu. Haiwezekani kumfunza kwa sababu maarifa yake hayana kikomo, tunaita hali hii anayejua. Hekima yote na maarifa hutoka kwake.

Nguvu na hekima hutiririka kwetu kwa Roho wake ambao ni kama mto.

> **Ufu 22:1** Kisha yule malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima, maangavu kama kioo yakitiririka kutoka kwenye kile kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo.

> **Zaburi 46:4,5** Kuna mto, vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu, Patakatifu pa maskani zake Aliye juu. Mungu yu katikati yake hautatetemeshwa; Mungu atausaidia asubuhi na mapema.

Kupitia kwa Roho wake Mungu anaweza kuwa kila mahali kwa wakati mmoja. Tunaita uwezo huu kila mahali. Tena, ni jambo ngumu zaidi kuelewa, lakini tunagundua kile ambacho Bibilia inasema:

> **Zaburi 139:7-10** Niende wapi nijiepushe na roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko; Ningefanya kuzimu kitanda changu, Wewe uko. Ningezitwaa mbawa za asubuhi, Na kukaa pande za mwisho za bahari; Huko nako mkono wako utaniongoza, Na mkono wako wa kuume utanishika.

Mto huu ni mto wa uzima, viambajengo vya uzima vinatoka kwa Roho na ni Roho wake apeanaye-uzima kwetu ambaye anatuweka hai na mioyo yetu ikidunda.

> **Matendo 17:24-28** "Mungu aliyeumba dunia na vyote vilivyomo ndani yake, Yeye ndiye Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono ya wanadamu. Wala hatumikiwi na mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji cho chote, kwa sababu Yeye mwenyewe ndiye awapaye watu wote uhai na pumzi na vitu vyote. Kutoka kwa mtu mmoja, yeye aliumba mataifa yote ya

> wanadamu ili waikalie dunia yote, naye akaweka nyakati za kuishi. Mungu alifanya hivyo ili wanadamu wamtafute na huenda wakamfikia ingawa kwa kupapasa – papasa ijapokuwa kwa kweli hakai mbali na kila mmoja wetu. ‘Kwa kuwa katika Yeye tunaishi, tunatembea na kuwa na uzima wetu’. Kama baadhi ya mashairi yenu yalivyosema, ‘Sisi ni watoto wake’

Hivyo katika muhtasari tunaona kuwa kuna Mungu mmoja ambaye ananguvu zote, hana mwisho katika maarifa na yuko kila mahali kwa Roho wake. Mamlaka yote na nguvu ni vyake na kwa yeyote ampae.

## 3. Hekima Ya Mungu

Itakuja kama mshangao kabisa kudhani kuwa kiumbe mwenye nguvu zote na mwenye hekima yuko katika nafasi ambayo hawezi fanya kitu. Kitu ambacho kilikuwa muhimu sana, bila kuwa nacho, Mungu Baba hangekuza ufalme wake.

Tunapoangalia maana ya ndani ya ukweli kuwa uzima wote, nguvu na hekima hutoka kwa Mungu, tunatambua kuwa Mungu hangeumba mamilioni ya wenyeji wa ulimwengu, awape orodha na kisha kuwaambia waifuate. Uwezo wa kumtii Mungu, kumwamini na kuhifadhi njia zake za kufanya mambo lazima ungekuwa sehemu ya mto ambao unatiririka kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu.

Tatizo ni kuwa Mungu hamtii mtu yeyote, wala hahitaji kumtii yeyote au kufuata njia zao za kutenda mambo. Katika hekima kuu, Mungu aliweza kumzaa Mwana kwa mfano wake halisi, akapeana kila kitu alichokuwa nacho kwa mwanawe na kisha akaumba kila kitu kupitia kwake. Tunagundua:

> **Ebr 1:1-5** Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu. Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza. Akiisha kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi aliketi mkono wa kuume wa Ukuu huko mbinguni. Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao. Kwa maana ni malaika yupi ambaye wakati wo wote Mungu alipata kumwambia, "Wewe ni Mwanangu, leo Mimi nimekuzaa?" Au tena, "Mimi nitakuwa Baba Yake, naye atakuwa Mwanangu?"
>
> **Yohana 5:26** Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake.
>
> **Yohana 5:19** Yesu akawaambia, Amin, amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, kwa maana lo lote afanyalo Baba, Mwana pia hufanya hivyo hivyo.

**Yohana 8:29** Yeye aliyenituma yu pamoja nami, hajaniacha, kwa kuwa sikuzote nafanya mapenzi Yake.''

**Yohana 8:42** Yesu akawaambia, ''Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa maana nilitoka kwa Mungu na sasa niko hapa. Sikuja kwa ajili Yangu mwenyewe, ila Yeye alinituma.

**Kol 2:8-10** Angalieni mtu ye yote asiwafanye ninyi mateka kwa elimu batili na madanganyo matupu yanayotegemea mapokeo ya wanadamu na mafundisho ya ulimwengu ambayo siyo ya Kristo. Maana ukamilifu wote wa uungu umo ndani ya Kristo katika umbile la mwili wa kibinadamu, nanyi mmepewa ukamilifu ndani ya Kristo, ambaye Yeye ndiye mkuu juu ya kila enzi na kila mamlaka.

Hakika kila kitu kilichohitajika kwa ulimwengu wa Mungu kiliishi ndani ya Mwanawe; nguvu, hekima, uzima lakini pia uaminifu na utiifu, kutambua mamlaka ya Baba na hisia za upendo wa Baba na kukubaliwa. Mwana wa Mungu ni ukamilifu wa Mungu mwenyewe na msingi dhabiti wa ufalme wa Mungu.

**Wafilipi 2:9-11** Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina, ili kwa Jina la Yesu, kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, vya duniani na vya chini ya nchi na kila ulimi ukiri ya kwamba YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Hivyo basi Baba alimuinua Mwanawe na akamfanya nguvu takatifu na mfano kwa ulimwengu. Mungu angesafirisha Roho wa Mwanawe katika maisha ya kila kiumbe alichoumba ili kuvipa uzima, hisia ya mibaraka na maarifa ya utiifu na kuamini kutii. Bila Roho wa Kristo haiwezekani kutii, kumwamini na kumtii Mungu. Gundua ambacho Bibilia inasema.

**Ufu 22:1** Kisha yule malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima, maangavu kama kioo yakitiririka kutoka kwenye kile kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo.

**Yohana 15:26** ''Lakini atakapokuja huyo Msaidizi nitakayemtuma kwenu kutoka kwa Baba, yaani, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, Yeye atanishuhudia Mimi.

**Rum 8:9,10** Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu. Mtu ye yote ambaye hana Roho

wa Kristo, yeye si wa Kristo. Lakini kama Kristo anakaa ndani yenu, miili yenu imekufa kwa sababu ya dhambi, lakini roho zenu zi hai kwa sababu ya haki.

Hii ndio maana Yesu anaitwa Hekima na nguvu ya Mungu. Utu wa Kristo unasafirishwa kupitia kwa Roho wa Mungu kupitia kwa ulimwengu kwa kila kiumbe kilicho umbwa. Ni hekima ya Kristo ambayo huja mioyoni mwetu ambayo hutufunza jinsi ya kumpenda na kumtii Baba; ni uzima ndio huhuisha kila neva na fiber za uwepo wetu na kutuhifadhi hai.

**1 Kor 1:24** Lakini kwa wale ambao Mungu amewaita, yaani, Wayahudi na Wayunani, Kristo ni nguvu na hekima ya Mungu.

**1 Kor 1:30** Mungu ndiye chanzo cha uzima wenu katika Kristo Yesu, aliyefanyika kwetu hekima itokayo kwa Mungu na haki na utakaso na ukombozi:

Kwa hivyo ni Roho wa Kristo katika ubinadamu ambaye huwapa hekima ya kufanya mambo na kuwa watakatifu na wema. Sulemani alizungumza kuhusu hili na jinsi hekima hutenda katika ulimwengu.

**Mithali 8:12-21** Mimi, hekima, nimefanya werevu kuwa kao langu; Natafuta maarifa na busara. Kumcha Bwana ni kuchukia uovu; Kiburi na majivuno, na njia mbovu, Na kinywa cha ukaidi pia nakichukia. Shauri ni langu, na maarifa yaliyo sahihi; Mimi ni ufahamu, mimi nina nguvu. Kwa msaada wangu wafalme humiliki, Na wakuu wanahukumu haki. Kwa msaada wangu wakuu hutawala, Na waungwana, naam, waamuzi wote wa dunia. Nawapenda wale wanipendao, Na wale wanitafutao kwa bidii wataniona. Utajiri na heshima ziko kwangu, Naam, utajiri udumuo, na haki pia. Matunda yangu hupita dhahabu, naam, dhahabu safi, Na faida yangu hupita fedha iliyo teule. Natembea katika njia ya haki, Katikati ya mapito ya hukumu. Niwarithishe mali wale wanipendao, Tena nipate kuzijaza hazina zao.

Kisha anaendelea mbele na kuelezea jinsi Mungu alimzaa na kumkuza Mwanawe.

**Mithali 8:22-31** Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. Nalitukuka tokea milele, tangu awali, Kabla haijawako dunia. Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa,

> Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Kabla milima haijawekwa imara, Kabla ya vilima nalizaliwa. Alipokuwa hajaiumba dunia, wala makonde Wala chanzo cha mavumbi ya dunia; Alipozithibitisha mbingu nalikuwako; Alipopiga duara katika uso wa bahari; Alipofanya imara mawingu yaliyo juu; Chemchemi za bahari zilipopata nguvu; Alipoipa bahari mpaka wake, Kwamba maji yake yasiasi amri yake; Alipoiagiza misingi ya nchi; Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake; Nikiifurahia dunia inayokaliwa na watu; Na furaha yangu ilikuwa pamoja na wanadamu.

Mshukuru Baba kwa Mwana, bila yeye ulimwengu hauwezi ukafanya kazi, hakuna chochote ambacho kinaweza tenda kazi vizuri. Hivyo sasa tunaona ukamilifu wa Uungu ukiletwa pamoja. Baba ni Mungu mmoja wa kweli ambaye ni chanzo cha vitu vyote. Alimzaa Mwana ambaye alimpa kila kitu. Kutoka kwa Kristo kunatiririka viambajengo vyote vinavyohitajika na ulimwengu ili kutenda kazi. Katika Mwana kuna nguvu na hekima vikiunganishwa na kuamina na utiifu. Utu wa Mwana unatiririka kwa ulimwengu kupitia Roho wa kila mahali wa Mungu. Ni mfumo wa kumetameta na Mungu anahekima kuu zaidi za kuuumba.

Paulo anafupisha hili kwa ajabu anaposema:

> **1 Kor 8:6** Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi.

## 4. Usawa

Katika sura iliyopita tulijifunza kuhusu hekima ya ajabu ya Mungu katika kuweka Msingi wa ulimwengu. Kumzaa Mwana aliyewekezwa sifa zake za Uungu kulitoa ukamilifu wa Mungu wa kusafirishwa mioyoni mwa viumbe vyote kupitia kwa Roho wa Mungu. Jambo lingine ambalo Mungu alilitenda lilikuwa kutoa kijelezi muhimu cha usawa wa viumbe vyote vya kimaadili, bila kuzingatia nafasi zao katika uumbaji.

Baba alimpa Mwanawe mamlaka ili awe sawa naye. Gundua kwa makini kwamba usawa wa Mwana haukuja kupitia kwa nguvu alizopewa, ila kupitia mamlaka ya Baba na mibaraka. Kama Mwana angefikiriwa tu kuwa sawa na Baba yake kwa sababu alimiliki nguvu zake, basi kijelezi cha usawa kinategemea usawa wa nguvu. Kijelezi kingemweka Mwana katika nafasi ya uwezo wa kupeana usawa wake kwa maonyesho ya nguvu zake. Hiki ndicho hasa Shetani alihitaji kutoka kwa Yesu jangwani; maonyesho ya nguvu kuthibitisha uhusiano wake na Baba yake. Kwa shukurani, Mwana anapumzika kwa ulimwengu wa Baba uliobarikiwa. Mwana anamwamini Baba tu na hana chochote cha kuthibitisha kwa mtu yeyote. Uhusiano wa Baba na Mwana ulifanyika kijelezi cha uhusiano wa ulimwengu. Uhusiano wote kati ya mpangilio wa viumbe ungefumwa kwa uhusiano wao. Baba alimfanya Mwanawe kuwa sawa naye.

> **Wafilipi 2:5,6** Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho,

> **Yohana 5:22,23** Wala Baba hamhukumu mtu ye yote, lakini hukumu yote amempa Mwana, ili wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Ye yote asiyemheshimu Mwana, hamheshimu Baba aliyemtuma.

Hatua hizi kwa hekima zilihakikisha kuwa kijelezi cha usawa kingekuwa katika wigo la mahusiano. Kwa hili tunamaanisha ni uhusiano unaoelezewa na Baba ambao unawafanya kuwa sawa. Alama zote za nguvu ambazo Mwana alirithi kutoka kwa Baba, na kwa hivyo haziundi sehemu ya kijelezi cha usawa. Zinaacha kuwa na thamani katika hesabu. Mungu alifanya hili ili kuhakikisha kuwa viumbe alioumba hawatajilinganisha kwa karama na

uwezo waliopokea, lakini badala yake kupitia kwa uwezo wao wa kujua na kuelewa kila mmoja.

Hali ya usawa wa Baba kwa Mwana ni ya namna ambayo inatoa kijelezi muhimu sana kwa ulimwengu. Tukiuelewa vibaya uhusiano huu, tutaelewa visivyo kiini hasa cha ufalme wa Mungu. Moja wapo ya vitu vya ajabu kumuhusu Mwana wa Mungu ni kwamba anajua kila kitu cha kujua kumhusu Baba. Hakuna mwingine kama yeye ambaye anaweza kuuwelezea ulimwengu jinsi Mungu alivyo. Tambua jinsi Yesu anaelezea usawa wake na Baba yake kwa namna ya mahusiano.

> **Yohana 10:15** Kama vile Baba anavyonijua Mimi, nami ninavyomjua Baba.

Kwa hivyo Yesu angesema kwa uhakika:

> **Yohana 14:9** Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema;

Huu sio baadhi ya ujumbe wa kipagani wa kiini kimoja; ni ujumbe kuwa Yesu anajua kila kitu kumhusu Baba yake na amejawa na tabia na utu wake. Hakuna mtu yeyote ulimwenguni ajuae mawazo ya Mungu sawa na vile anavyojua mawazo ya kila mtu – Mwana ni yeye tu. Uhusiano wao unahakikisha kuwa kile tunachoabudu ni uhusiano wa kweli kati yao badala ya nguvu wanazomiliki pamoja.

Nabii Yeremia anadhihirisha utukufu wa ufalme wa Mungu aliposema:

> **Yer 9:23,24** Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana.

Hivyo basi tunapata kuwa kijelezi cha usawa kinachoweka toni yote ya ufalme wa Mungu kimejengwa katika utambulisho hasa wa Baba na Mwana na jinsi wanavyohusiana. Mgao wa nguvu wa Mwana na Baba hauamuliwi na chochote ambacho yeye anaweza leta kwa namna ya nguvu na nafasi, lakini tu kwa mapenzi na radhi ya Baba.

**Wafilipi 2:9** Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina,

**Ebr 1:6** Tena, Mungu amletapo mzaliwa Wake wa kwanza ulimwenguni, husema, “Malaika wote wa Mungu na wamsujudu.”

**Luka 9:35** Sauti ikatoka kwenye lile wingu ikisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, msikilizeni Yeye.”

Usawa umejengeka kwa msingi wa mamlaka ya Baba, sio kwa sifa za Mwana wake. Ndani ya kijelezi hiki Baba na Mwana wanadumisha utambulisho wao binafsi, ila wako sawa.

Athari za hili zinaweza kosa kuonekana dhahiri mwanzoni, lakini athari zake kwa familia ya mwanadamu ni kubwa sana, hasa wakati tunazungumza kuhusu usawa kati ya wanaume na wanawake na kile kinachouelezea.

## 5. Mapenzi

Sasa tunaona kwamba Roho wa Mwana wa Mungu anatiririka kwa wenyeji wote wa ulimwengu na anaishi ndani ya mioyo na mawazo ya wote. Ili ulimwengu wa Mungu kuwa na mahusiano ya kweli, viumbe alioumba walifaa kuwa na uwezo wa kuchagua kukubali au kukataa Roho huyu apeanaye uzima wa Mwana. Bila nguvu hizi za kuchagua, uumbaji wote unaweza kuachwa ujiendeleze wenyewe na kuwa wa kiroboti kabisa. Mungu amempa kila kiumbe wa kimaadili mapenzi na nguvu za kuchagua. Nguvu za kuchagua zimefungwa kwa chaguo moja: kumpenda Mungu na kumkubali na Roho wake apeanaye uzima kupitia kwa manawe au kukataa uzima wake na kujiletea maafa kwetu wenyewe.

> **Yosh 24:15** Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.
>
> **Mit 3:5,6** Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.

Nguvu za kuchagua humaanisha kuwa kila mmoja anachukua umiliki wa tabia ya upaji uzima ya Mwana wa Mungu. Upendo wa Mwana kwa Baba unakuwa upendo wetu; kutii na kuamini kwa Mwana wa Mungu kunakuwa kutii kwetu na kuamini. Haki yake inakuwa yetu, kuchagua kutii daima. Uwezo wa kutii na kuchagua kiasili ulifanyika bure kupitia kwa mto, lakini kama tutakavyo ona katika sura ijayo, mgogoro ulikuja ulimwenguni ambao ulidakiza familia ya Mungu na ukaleta maumivu makuu kwa wote.

## 6. Mgogoro Unazuka

Kwa uwepo wa kila kitu, Mwana wa Mungu alipewa kazi ya kuumba ulimwengu. Kupitia kwa nguvu za Baba yake, Aliumba jeshi lake lote, sayari na viumbe hai vyote. Aliumba malaika wengi, wa kwanza akiwa ni Lusifa – nyota ya asubuhi.

> **Yohana 1:1-3** Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna cho chote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa
>
> **Efe 3:9** kuweka wazi kwa kila mtu jinsi ile siri iliyokuwa imefichwa kwa nyakati zote katika Mungu aliyeumba vitu vyote.
>
> **Ebr 1:1,2** Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu.

Lusifa alijua nafasi ya Mwana wa Mungu na kuwa amepokea utimilifu wote wa Mungu Baba kama urithi. Alianza kupoteza mtazamo wa hekima ya Mungu katika Mwanawe. Kupitia kwa karama ya mapenzi, alianza kuswali ni kwa misingi ipi Mwana wa Mungu anakuwa sawa na Mungu. Alianza kutamani nafasi ya Mwana, na kujadili kuwa kama Mwana anaweza pokea nafasi hii basi mbona basi naye asiwe nayo pia? Mbona kusiwe na kiumbe wa tatu tofauti ambaye atakuwa kama Mungu? Hakuelewa jukumu muhimu la Mwana na Roho wake wa utiifu ulioshikamanisha ulimwengu wote pamoja. Kol 2:9,10.

Badala ya kukumbatia utambulisho na tabia ya Mungu na Mwanawe, alianza kutamani nguvu na nafasi ya Mungu. Moja wapo ya msatari wa kuwaza alioufikia ulikuwa kama Mwana alikuwa wa pekee kwa Mungu basi Mungu hangekuwa sawa. Alishangaa ni jinsi gani angeabudu kiumbe ambaye hana nguvu za kiasili na alimiliki uwepo wake kwa mtu mwingine. Alifikia hitimisho kuwa pengine aruhusiwe kufurahia hadhi sawa kama Mwana au ataifikiria kuwa wizi kwake kwa Mwana kufanywa kuwa sawa na Mungu.

**Wafilipi 2:5,6** Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho.

**Isa 14:12-14** Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu.

**Eze 28:14,15** Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako.

Lusifa alisema moyoni mwake kuwa ataanzisha utawala wake juu kuliko nyota za Mungu. Atainuka juu afanane na yeye aliye juu. Lengo lake lilikuwa kupata nguvu na nafasi. Hakuwa na hamu ya tabia ya Mungu, nafasi yake na nguvu tu.

Ni ajabu jinsi Lusifa alianza kuwaza jinsi hii. Bibilia haituambii, lakini kwa sababu Mungu aliwapa viumbe wote nguvu za uchaguzi, Lusifa alitumia nguvu hizi kugeuza moyo wake mbali na hekima ya Mungu na utiifu kwake na mpango wake kwa ulimwengu.

Mungu alijaribu kusemezana na Lusifa kuhusu mwelekeo aliokuwa akifuata. Alielezewa mbona Mwana wa Mungu alishikilia nafasi aliyokuwa nayo. Lakini Lusifa alikataa kusikiliza na akawa Shetani – mshitaki. Alimshitaki Mungu kwa kuweka ufalme mbaya na akakataa kumwabudu Mwana wa Mungu. Alichagua badala yake kuamua kuwa kama hatakuwa sawa na Mungu basi angemkubali Mungu ambaye ana nguvu zake mwenyewe asilia na hakuzipokea kutoka kwa mtu mwingine.

Kuna hoja muhimu zaidi ya kuundwa hapa. Mungu pekee ndiye chanzo cha uzima. Kutokukubaliana na Mungu na kukataa kumwamini na kumtii mara moja hukukata kutoka kwa uzima wako. Uzima huja kwetu tu katika kutii

Mungu na utiifu huja kwetu tu kupitia kwa Roho wa Mwana. Hii ni moja ya sababu kadhaa ya mbona Baba na Mwana wote ni Muhimu. Kwa kukataa kutii, Luciefer alikuwa akikataa Roho wa utiifu wa Mwana. Kitendo hasa cha upinzani ni kitendo cha chuki na mauaji. Hii ndio maana mawazo ya kidunia ni uadui kwa Mungu. Rum 8:7. Shetani alipompinga Mungu, Mungu mara moja lazima angefanya uamuzi – uamuzi ambao alijiandaa kwao, lakini sasa lazima utekelezwe. Kwa kumpinga Mungu, Luciefer alikuwa akisema hapana kwa Roho wa Kristo, alikuwa akimuua Mwana wa Mungu. Alikuwa akisema nataka nguvu zako, lakini sio Mwanao. Aidha Mungu angemwacha shetani afe mara moja kwa kuacha chanzo cha uzima kiondoke au angemruhusu Mwanawe afe kulingana na kile ambacho Lusifa alikuwa akikifanya mawazoni mwake. Kifo cha Yesu sio kitendo cha haki ya mahakama kwa upande wa Mungu kulipiza kisasi halisi; ni kudhihirisha sheria asili ya ulimwengu kwamba uzima hutoka kwa Mungu na Mwanawe tu. Lusifa hangefaidika kutokana na kifo hiki kwa sababu hakuchagua kukubali utambulisho wa Mwana wa Mungu; lakini kifo cha Yesu kinagharamia kampeni yote ya Shetani na malaika wake ili kwamba ulimwengu uone kilichokuwa mawazoni mwa Shetani. Kama Lusifa Shetani angekufa badala ya Mwana akichukua uwamuzi tangu mwanzo, hakuna mtu yeyote angeelewa mbona Mungu angeogopwa badala ya kupendwa. Mwana wa Mungu alishikwa katika treni ya mizigo ya upinzani wa mapenzi ya Mungu. Aidha Mungu angefuta treni au amruhusu mwanawe afe, katika matumaini kuwa tutakuja kumjua yeye kweli ni nani. Hili ndilo ambalo kifo cha msalaba kinahusu hakika – kujua utambulisho wake wa kweli katika ufalme wa Mungu Yohana 17:3.

Shetani alianza kueneza maoni yake kwa malaika wengine na hatimaye theluthi moja ya malaika walidhani kuwa Lusifa alikuwa sawa. Mbona wamtii Mwanawe ambaye alirithi kila kitu kutoka kwa Baba, ni nini kilikuwa cha kipekee kumhusu? Walikataa kutii mapenzi ya Mungu. La kuhuzunisha, vita vya maneno [*polēmos*] vilianza mbinguni na Shetani na wafuasi wake walifukuzwa.

> **Ufu 12:7-9** Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka pamoja na malaika zake likapigana nao.

> Lakini joka na malaika zake wakashindwa na hapakuwa tena na nafasi kwa ajili yao mbinguni. Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake.

Mungu angemwacha Shetani afe, lakini mbegu kamili ya kufikiria kwake hatari ilihitaji kuruhusiwa kuwa wazi. Shetani alipokuwa amekataa uzima pekee uliokuwepo kwake kupitia kwa Mwana wa Mungu, angeweza kuruhusiwa aangamie, lakini malaika na wengine ulimwenguni wangeanza kufikiria kuwa Mungu kwa kweli alikuwa amemwangamiza kwa nguvu na kuelekea kwa uongo kuwa Mungu kiasili ni mkatili. Kila mtu angejifunza mwenyewe mbona maisha yanawezekana tu kwa uumbaji kupitia Mwana. Kila mtu ulimwenguni angekuwa na fursa ya kuamua nani alikuwa sawa; Mungu au Shetani.

## 7. Aliumba kwa Mfano Wake

Shetani na theluthi ya malaika walikuwa wameswali nafasi ya Mwana na uhusiano wake kwa Baba yake. Hakuna yeyote aliyekuwepo kuthibitisha mwanzo wa uhusiano wa Baba na Mwana na kwa hivyo walihitajika kumwamini Baba kuwa alijua kilichokuwa bora kwa kila mtu.

Akijua kuwa ungekuja wakati ambao uhusiano wake na Mwanawe ungewekwa katika maswali, Mungu alikuwa ameweka tayari mpango wa kuelezea kikamilifu zaidi uhusiano wa kipekee aliodumisha na Mwanawe. Angetoa mfano kwa ulimwengu kutazama kwa ukaribu mienendo muhimu ya uongozi na utiifu katika uhusiano wa Baba-Mwana.

Kwa kweli wakati Baba na Mwana walikuwa wakipanga mradi wa dunia kukatishwa tamaa kwa Lusifa hakika kuliongezeka. Lusifa alikuwa ametamani kuwa mkuu wa ulimwengu huu kwa kuwa ulimwengu huu ungeumbwa kwa mfano wa Baba na Mwanawe. Lusifa akawa mwenye wivu kwa Mwana wa Mungu. Kama tu Lusifa angeamini kuwa mradi huu ungemsaidia kwa ubora kuelewa uhusiano wa kipekee kati ya Baba na Mwana na mbona jukumu la Mwana lilikuwa muhimu katika ufalme wa Mungu. La kuhuzunisha, hili halingekuwepo.

Mungu na Mwanawe waliendelea na mpango wa kuumba dunia na kudhihirisha kwa ulimwengu mfano wa kipekee wa uhusiano wao. Na Mungu akasema kwa Mwanawe “Natumfanye mtu kwa mfano wetu.” Mwa 1:26.

Ni nani anaweza fahamu upana wa ubunifu uliotendeka katika juma la uumbaji! Siku baada ya siku, kama nguvu za ubunifu za Mungu zikitoka kwa Mwanawe, ulimwengu ulichukua sura. Nchi, nyasi na maua, miti, jua na mwezi, wanyama, jukwaa lilipangwa kwa mnara wa uumbaji – uumbaji wa mwanamume na mwanamke.

Mchakato wa uumbaji ni muhimu sana na unatwambia kisa muhimu kumhusu Mungu na Mwanawe.

> **Mwa 1:27** Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.

Huu ni mchakato wa jinsi ilitendeka.

> **Mwa 2:7** Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.

> **Mwa 2:18-25** Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake. Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya.

Mungu, kupitia kwa Mwanawe, alimfanya Adamu kutoka kwa mavumbi ya ardhi, na kisha mto wa uzima ulitoka au ulipulizwa ndani yake. Sifa za thamani za Mwana wa Mungu, ziitwazo hisia za mibaraka ya Baba na upendo wa imani na utiifu wa Mwana, zilipitishwa kwa furaha kupitia hiari ya Adamu na ikawa sehemu yake. Adamu kiasili alitamani kumtumikia Mungu na kumpendeza, kwa sababu alikuwa akipokea hamu hii kutoka kwa Mwana wa Mungu kupitia kwa Roho.

> **1 Kor 2:16** “Kwa maana ni nani aliyejua nia ya Bwana ili apate kumfundisha?” Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.

Mungu alimweka Adamu katika hali ambayo angeanza kujifunza kuwa alikuwa anakosa kitu. Mbona Mungu angemuumba Adamu na kumuongoza tu kupitia mchakato kuwa alikosa kitu? Hili linatufunza jambo la kuvutia kumhusu Mungu na ufalme wake: baadhi ya vitu vinaweza tu somwa

kupitia tajriba, na kwa Adamu utambuzi kuwa kitu kilikuwa kinakosekana ulizidisha hamu yake kwacho na hisia refu ya kushukuru Mungu alipompa.

Adamu alikosa rafiki ambaye angeelewa mawazo yake na fikira; mtu ambaye angethamini furaha yake na kuelewa anachopitia. Adamu alipowapa wanyama majina alianza kutambua hakuna aliyekuwa kama yeye, hakuna wa kumuelewa. Hisia hii ilitia katika Adamu kile kilichokuwa msingi wa ufalme wa Mungu: uhusiano wa karibu. Inaleta maana kuwa njia ya pekee ya kulielewa ni kulishuhudia. Mungu angeweza kumwambia Adamu umuhimu wa uhusiano na kuelezea uzuri wake, lakini katika kumpa adamu zoezi la kuwapa wanyama majina, ilikuja wazi haraka sio kwa akili ya Adamu tu, bali pia kwa moyo wake, ambalo lilikuwa muhimu.

Mbona Mungu alimtia Adamu usingizi na kufungua mwili wake na kutoa umbavu uliohai na kumfanya mwanamke kutoka kwao? Hili halionekani kama njia ngumu ya kufanya mambo? Mchakato ni mafunzo ya juu. Mchakato wa Hawa kutoka kwa Adamu, akiumbwa kutoka kwa sehemu yake na kutoka kwa upande wake karibu na moyo, inazungumza moja kwa moja kwa kisa cha Baba na kumtoa Mwanawe. Mbona Mungu hakuchukua sehemu ya ubongo wa Adamu, mbona ilikuwa umbavu ambao ulikuwa juu ya moyo? Bibilia haituambii mbona, lakini inanizungumzia kuhusu azimio la uchungu ambao ulikuwa moyoni mwa Adamu kutokana na kukosa rafiki ambaye angemwelewa na kumhudumia kama wakala wake mtiifu wa kumlea kwa mbegu aliyokuwa amebeba.

> **Yohana 1:18** Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha.
>
> **Yohana 8:42** Yesu akawaambia, ‘‘Kama Mungu angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa maana nilitoka kwa Mungu na sasa niko hapa. Sikuja kwa ajili Yangu mwenyewe, ila Yeye alinituma.
>
> **Mit 8:23-25** Nalitukuka tokea milele, tangu awali, Kabla haijawako dunia. Wakati visipokuwako vilindi nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji. Kabla milima haijawekwa imara, Kabla ya vilima nalizaliwa.

**Warumi 1:19,20** kwa maana yote yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao. Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani, uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru.

Katika mafungu ambayo tumeorodhesha, tunaona ushahidi ambao unaonyeshwa wa Mwana wa Mungu kuja kutoka kifuani mwake. Neno aliendelea na kuja linamaanisha "kutoka nje ya" na Mit 8:25 inazungumza moja kwa moja kwa kuzaliwa. Mtume Paulo akitoa maoni kuhusu hili anasema kuwa uumbaji unatupa taswira ya moja kwa moja ya Baba Mungu tusiwe na udhuru.

Nani anaweza kufikiria ambacho Adamu aliwaza alipomuona Hawa mara ya kwanza, macho yao yalipokutana na utambuzi ukamjia kuwa hapa kulikuwa na mtu ambaye kwa kweli angemuelewa na kumthamini. Mtu ambaye alikuwa kiini chake na mtu ambaye angebeba mbegu yake, ailee, na kuwa wakala muhimu mtiifu ambaye alihitaji kuwaonyesha wanawe na wajukuu umuhimu wa kusalia mtiifu. Kama Mungu alivyohitaji Mwanawe kutoa tabia hii ya utiifu, Mungu aliweka ufalme wa duniani ili kwamba mwanaume hawezi jenga ufalme bila mke wake. Wanawake hawawezi jua jinsi ya kutii bila mfano hai katika namna ya mama.

Kuna utakatifu mkubwa ambao upo kati ya mume na mke. Uhusiano huu unapowekwa kwa usahihi unanena moja kwa moja kuhusu uhusiano wa Baba na Mwana na ni ukumbusho wa daima kwa ulimwengu wa madai ya uongo ya Shetani kwa Mwana wa Mungu.

**1 Kor 11:10** Kwa sababu hii na kwa sababu ya malaika, mwanamke inampasa awe na ishara ya mamlaka iliyo juu yake.

Mungu alibuni uhusiano wa mume na mke kuwafundisha malaika kuhusu uhusiano wa Baba na Mwana. Ni karama ya ajabu namna gani kuumba kwa kusudi hili.

Tukijua ukweli huu, tunaweza pata kwamba siri hasa ya ndoa ni katika kuruhusu nafsi zetu kuvutwa na Roho wa Mungu kwa mfano wa uhusiano

wa Baba na Mwana; mume akitenda kama chanzo cha mibaraka na mke akitenda kama onyesho hai la imani ya kupenda na kutii.

Adamu na Hawa walipewa wito wa juu na wa furaha. Kama tu wangedumu katika mfano wa Baba na Mwana, ni taabu ngapi zingeondolewa.

## 8. Baba wa Uongo

Tunakumbuka kwamba Shetani alikuwa ameamua kuwa kama Mungu hangemruhusu kuwa na fursa ya kufikia nguvu na fadhila za Mwana wa Mungu basi angehitimisha kwamba angemwabudu Mungu mwenye nguvu asili ambazo haziwezi rithiwa. Baada ya Mungu kukataa kukubali "mageuzi" ya Shetani, Shetani aliwekwa katika nafasi ya kukiri kuwa bado alikuwa na deni ya maisha kwa Baba, hata kama hangekiri nafasi muhimu ya Mwana.

Hakukuwa njia yoyote kwa Shetani kuanzisha ufalme kwa msingi wa kanuni zake kama hakuwa akitambua kila wakati kuwa nguvu zote hutoka kwa Mungu. Hivyo alizuka na UONGO MKUBWA – kila mtu ana uzima ndani yake. Kulikuwa na chaguzi kadhaa za kuamini jinsi hii. Unaweza amini kuwa hautakufa tu na umilele ni sifa ya kiasili ya kila kiumbe. Unaweza amini kuwa maisha yapo tu kama nguvu na kila mtu ameunganishwa kwayo na anaweza itumia kufanya atakacho. Au unaweza kumwamini Mungu ambaye amekupa karama ya umilele uitumie kwa ubora wa uwezo wako. Haikujalisha uchaguzi ambao uliuchukua, mradi tu uliamini kuwa ulikuwa na chanzo cha uhai chako wewe mwenyewe. Huu ni uongo mkubwa ulimwenguni. Kama Yesu alivyosema:

> **Yohana 8:44** Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo.

Mungu angeweza kumaliza uongo huu mara moja kwa kuruhusu waliomkataa Mwanawe kuisha, lakini Mwana aliendelea kuwakirimia uzima ingawa ulikuwa mchungu kwake. Ili ulimwengu uone athari za uongo, Mwana lazima angebeba malaika walioanguka na kuwasambazia maisha hata wakati walitamani kumuua na kumwangamiza. Shetani na malaika zake walipomkataa Yesu, hawakupokea tena roho wa kuamini utiifu na kutii ambaye hutoka kwake pekee. Walijisurubishia Mwana wa Mungu katika tabia yake na Roho ila Mungu aliendelea kuwapa nguvu za uzima ili shetani awe na wakati wa kuonyesha falsafa yake, Mungu alifanya hili ili ulimwengu uamue, alijua jinsi bora. Kama tulivyotaja awali, kulikuwa na gharama ya

kuruhusu shetani kumpinga Mungu – iligharimu uhai wa aliyekataliwa na huyo ni Mwana wa Mungu. Shetani alikuwa muuaji tangu mwanzo; alisababisha kifo cha Kristo katika upinzani wake kwa Mungu. Kifo hiki kilikuwa kikitendeka mawazoni mwa Shetani, na hili lingehitaji kuwekwa wazi kwa ulimwengu kwa kila mtu kuona kilichokuwa kikiendelea. Hayakuwa mapenzi ya Mungu udhihirisho huu kutendeka duniani, lakini kwa huzuni hapa ndipo ungetendeka.

## 9. Wanadamu Kudanganywa

Katika sura iliyopita tuliona sehemu muhimu ya nia. Karama ya nia imepewa wanaume na wanawake kuwaruhusu kuchagua kumnyenyekea Mungu. Bila uwezo wa kuchagua kunyenyekea hakuna baraka za kweli au hisia za kumpendeza Baba ambaye analeta baraka. Tazama kile Yesu anachosema:

> **Yohana 8:29** Yeye aliyenituma yu pamoja nami, hajaniacha, kwa kuwa sikuzote nafanya mapenzi Yake.

Yesu alikuwa mara kwa mara na hisia za Baraka kupitia kwa kila saa kunyenyekeza nia Yake kwa nia ya Baba. Karama ya nia inaleta mibaraka mingine zaidi ya hii, lakini hiyo nikusema zaidi ya masomo haya. Wakati Mungu alipomuumba Adamu na Hawa, Ilibidi awapatia njia ya kufanyia mazoezi nia yao. Ilimbidi awape uchaguzi. Bila uwezo wa kuchagua kutompendeza, hakuna uwezo wakupokea baraka za kumpendeza.

Mungu aliumba uwezo wa kumpendeza kwa kupeana uhuru wa kumkana kwa kula katika mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

> **Mwa 2:16,17** Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.

Kwa kuchagua kila siku kutokula kutoka kwa mti huo wa kipekee, Adamu na Hawa walipata baraka za kipekee za unyenyekevu; hisia kwamba Mungu alipendezwa nao. Bila mti huu kuwa hapo, hawangepokea Baraka hii.

Ijapokuwa Shetani alitolewa mbinguni, alipewa fursa ya kuingia duniani kwetu kwa sehemu moja ambapo uchaguzi wa kutompendeza mungu ungefanywa usisimke. Hapa ndipo tunampata Shetani akichukua mfano wa nyoka akapanda mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Tunajua nyoka huyu ni Shetani kutoka kwa kitabu cha ufunuo.

> **Ufu 12:9** Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake.

Kwa yale tumejifunza kuhusu mtazamo wa Shetani wa maisha, kwa kutakujishindia Adamu na Hawa kwa ufalme wake angewaonyesha mtazamo wakupata uhai ambao utatoa haja ya kumtegemea Mungu. Tazama kile Shetani anasema:

> **Mwa 3:1-5** Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa. Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.

Shetani alishauri kwamba kutompendeza Mungu kwa kukataa amri zake Alizoamuru hakungeleta laana bali baraka; macho yao yatafunguliwa kupata elimu kuu na hekima na watakuwa kama miungu hao wenyewe. Alisema kwamba hawatakufa, ambayo inamaanisha kwamba wangeendelea kuishi bila kumtegemea Mungu. Wangejiamini wao wenyewe na hukumu yao.

Ni huzuni ya namna gani kwamba Hawa alichukuwa mawaidha ya nyoka, tena akamwendea Adamu akamshinikiza kutomuamini Mungu na uongo mkubwa wa Shetani. Wakati walipokula tunda hili na kuamini uongo, mtazamo wao wa Mungu ukabadilika kabisa, wao wenyewe na vile ulimwengu ulivyo.

Kwa kuamini uongo, Adamu na Hawa walisonga mbali na imani ya kwamba vitu vyote vinatiririka kutoka kwa Mungu. Walikataa wazo la kwamba furaha yao ilitegemea kuamini na kunyenyekea kwa Mungu. Kwa kukataa amri za Mungu waliua tabia nzuri zaidi ya Mwana wa Mungu- utifu wa imani na kunyenyekea. Ilimbidi Mungu awaonyeshe Adamu na Hawa kwamba kukoma kunyenyekea kwa Mungu ni kwa hakika mashambulizi kwa Mwana Wake na kile alichosimamia. Adamu na Hawa walimuua Mwana wa Mungu katika fikira zao kwa kukataa roho ya unyenyekevu, ambayo ni Roho ya Mwana wa Mungu. Hiki ni kidokezi muhimu cha kuelewa. Tendo la kumuasi

Mungu ni tendo la kuua Roho wa Mwana Wake, kiini cha unyenyekevu. Hii ndio maana Yesu alimuita Lusifa mwuaji tangu mwanzo.

> **Yohana 8:44** Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo.

Malaika wote ambao walimkata Mwana wa Mungu na kugeuka kwa chuki kumhusu walimuua katika fikira zao. Bibilia inasema wazi kwamba kuna kiungo kati ya chuki na mauaji.

> **1 Yohana 3:15** Yeyote amchukiaye ndugu yake ni mwuaji, nanyi
>
> mwajua ya kwamba mwuaji hana uzima wa milele ndani yake.

Kafara ya Mwana wa Mungu ilionekana kabla ya ulimwengu huu kuumbwa. Njia mmoja tu ambayo uliwengu ungeelewa kile kilichokuwa katika fikira za malaika walioasi ni kwa kuacha kidhihirike. Tazama:

> **1 Petero 1:19,20** Bali kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ile ya Mwana Kondoo asiye na dosari wala doa. 20 Yeye aliwekewa hayo kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu, lakini akadhihirishwa katika siku hizi za mwisho kwa ajili yenu,

Mungu hakupatikana kighafula kwa uasi wa Shetani, alijitayarisha; Baba na Mwana walishauriana mpango wa wokovu, lakini uasi wa Shetani ulifanya kwa hakika hitaji la kukamilisha mpango huo. Wakati alipolia "Nitapaa mbinguni na nitakuwa kama aliye juu" Hakukuweko na makao kwa Mwana wa Mungu katika huo mpango; ilibidi atupwe na aangamizwe.

Shetani alipitisha uasi wake kwa kizazi cha binadamu na Mwana sasa atawajibika kuwafia. Kristo atadhihirisha kwa ulimwengu wa kimaumbile kwamba wanadamu walimuua Mwana wa Mungu mnyenyekevu katika fikira zao. Ilibidi ifichuliwe iliionekane kwa wote. Hiyo ndiyo moja ya sababu Musa aliamriwa kuweka nyoka mtini; tendo la kusulubisha lilikuwa nikufichua muundo wa mauaji ya Shetani. Hangeweza kuficha kusudio lake dhidi ya Kristo.

Kwa hivyo Adamu na Hawa walipo tenda dhambi na kukana Roho wa Kristo wa unyenyekevu, walikuwa na hatia ya mauaji pamoja na Shetani. Kristo aliuliwa katika mawazo ya Adamu na Hawa.

> **Ufunuo 13:8** Nao watu wote waishio duniani watamwabudu huyo mnyama, yaani, wale wote ambao majina yao hayakuandikwaa kwenye kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangukuumbwa kwa ulimwengu.

> **Ebr 6:6** kisha wakaanguka, kwa kuwa kwa nafsi zao wanamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili na kumfedhehi hadharani..

Tendo hili la kumuua Mwana wa Mungu lilipewa Adamu na Hawa kama ishara kwa tendo lifuatalo.

> **Mwa 3:21** Bwana Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.

Mavazi ya ngozi yalitoka kwa wanyama. Ilibidi hawa wanyama wachinjwe ilikuwavisha Adamu na Hawa. Adamu na Hawa hawakuhitaji nguo mpaka walipotenda dhambi. Walikuwa wamevishwa utukufu wa Mungu, lakini walipomkataa, walipoteza utukufu. Kumchinja mwana kondoo ilikuwa ni mfano wa ahadi ya Mungu kumtuma Mwana Wake ili kwa hakika awaonyeshe kile walicho kitenda katika fikira zao. Ili kuwasaidia kuona vile kumkana Mungu ni jambo baya; laana mbaya inayokuja tukikataa kunyenyekea. Inafanya mtenga Mwana wa Mungu – kiini cha unyenyekevu.

> **Mwa 3:15** Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

> **Yohana 1:29** Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, "Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!

Ni jambo la kushangaza Mwana wa Mungu angejitoa kufanya. Angelionyesha ulimwengu kukataa unyenyekevu kunafanya, kunauwa Roho wa mtu mwenye thamani ambaye Baba anampenda – Mwana Wake. Mwana wa Mungu alijibu msiba wa kukana kwa unyenyekevu wa maajabu. Dhihirisho la nguvu kwamba dunia haingeweza kubaki vile ilivyokuwa. Ingeonyesha ulimwengu vile Mwana wa Mungu ana thamani na kwamba tumpende na kumkubali na kufahamu Roho Wake wa unyenyekevu kwa Baba na amri zake.

## 10. Muhtasari

Tumefuatilia kwa uangalifu kutoka kwa Bibilia kile ambacho Mungu anafunua kuhusu Yeye Mwenyewe hapo mwanzo. Tumejifunza kwamba:

1. Kuna Mungu Mmoja wa kweli anayeitwa Baba. Yohana 17:3; 1 Wakorintho 8:6; 1 Tim 1:17
2. Yeye ndiye chanzo cha uhai wote na Baraka. Yakobo 1:17
3. Alileta Mwana kwa mfano wake na akampa uwezo wote na akamfanya sawa na Yeye. Ebr 1: 1-5,; Mithali 8:12 – 30 ;Wafilipi 2:6; Yohana 5: 26; 8:42; Wakolosai 2:9
4. Mwana wa Mungu ndiye ufunguo wa ufalme wa mbinguni. Ana viungo muhimu vya utiifu wa kuamini na unyenyekevu na baraka. Math 3: 17, Zabu 40: 8; Yohana 8:29.
5. Roho wa Mwana anatirirka kwa ulimwengu na anaishi ndani ya wale ambao wamechagua kunyenyekea kwa amri za Baba. Ufun 22: 1,2; Yohana 7: 37, 38; Waru 8: 9,1
6. Lusifa, malaika wa kwanza kuumbwa, alikataa utambulisho wa Mwana wa Mungu na akakataa kutii agizo la Mungu la kumwabudu. Yohana 5:22; Wafilipi 2:6; Rev 12:7-9; Ebr 1:6
7. Lusifa alikuwa Shetani na akachukua theluthi moja ya malaika katika kuamini kupya kwamba hakuna haja ya kunyenyekea kwa Mungu kwa sababu tuna uhai ndani yetu. Ufu 12:4, Mwa 3: 4,5.
8. Tendo la kukataa amri za Mungu ni sawa sawa na kumuuwa Mwana Wake - kiini cha unyenyekevu, amini, utiifu. Yoh 8:44; Ufu 13:8; 1 Yohana 3:15

9. Mwana alinyenyekea kwa mpango wa Baba Yake kuonyesha ulimwengu vile upinzani ulivyomfanyia Mwana Wake, kwa kumtuma ili atufilie. Mwa 3:15; Ebr 6:6.

Sasa tumepeana Picha wazi ya Bibilia ya Mungu, Mwana Wake na Roho zao, na vile wanavyofanya kazi. Pia tumeanzishiwa uongo wa Shetani kuhusu pahali uhai unapotoka na roho ya upinzani. Sasa tufuatilie hatua za mwanzo wa desturi hizi mbili ambazo zimekuzwa hapa duniani.

## 11. Njia Mbili

Katika sura za hapo awali, tulichunguza tofauti muhimu ya mawazo kati ya Mungu na Shetani.

Ufalme wa Mungu ulianzishwa kuonyesha utakatifu wa uhusiano; Ufalme wa Shetani unaangazia upatikanaji na uwezekano wa uwezo.

Ufalme wa Mungu unafanya kwa Baraka kupitia unyenyekevu, kuamini na kutii; Ufalme wa Shetani unafanya kwa kupitia "Baraka" kwa upinzani na uhuru kutoka kwa mamlaka ya Mungu.

- Ufalme wa Mungu unaelezea usawa kwa uwezo wa kumjua mwengine; Ufalme wa Shetani unaelezea usawa kwa uwezo, cheo, mafanikisho kwa kupitia uwezo wa kiasili.
- Ufalme wa Mungu unaongozwa kwa kupitia muundo wa kifamilia na wanachama wa ufalme wanalazimishwa na upendo; Ufalme wa Shetani unaongozwa kwa kupitia anuwai tofauti ya muundo wa mamlaka na wanachama wa ufalme wanalazimishwa kwa udhalimu.
- Ufalme wa Mungu unaelezea thamani kwa tabia na uhisiano; Ufalme wa Shetani unaelezea thamani kwa uwezo.
- Tofauti inaelezewa hivi kwa muhtasari kwa aya ya Bibilia inayofuata:

> **Yer 9:23,24** Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; 24 bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana

Tukitazama historia, tutaona yakuwa mtazamo wa wanadamu wa Mungu umegawanyika kwa njia hizi. Saa zingine ni vigumu kutambua kanuni inayofanya kazi kwa sababu Ufalme wa Shetani unatumia uhusiano kupata uwezo na lugha inaweza kuonyesha uhusiano, lakini bado inalenga uwezo.

Kama vile Shetani alivyomshawishi Hawa, kukubali imani kwamba tuna uhai ndani yetu na inafanya asili yetu kuwa ya miungu. Kwa mtazamo huu, mawazo ya watu kuhusu Mungu huwa ni kwa kweli huwa ni makadirio ya tabia ya wanadamu na uwezo. Hili linaonekana wazi katika hadithi za

kiyunani na maelezo yake kuhusu Zeus – Mfalme  wa miungu; Aphrodite – mungu wa upendo na urembo; Apollo – mungu wa muziki, dawa, afya; Ares mungu wa vita. Hii ni miungu ambayo ni uainishaji tu wa tabia ya wanadamu na kiini cha kujiabudu, kujiainisha, iliyoahidiwa na Shetani kwa Hawa katika Shamba la Edeni.

Ningependa tuanze historia yetu kwa kulinganisha watu wawili katika Bibilia ambao wanapeana mifano bora katika mifumo miwili: Ibrahimu na Nimrodi.

## 12. Msingi wa Babeli

Kabla hatujaangazia moja kwa moja hadithi ya Ibrahimu na Nimrodi, tutaangalia kwa muhtasari historia inayotuelekeza wakati huo.

Tuliona ya kwamba tunda la kwanza la kukumbatia uongo ni Hofu. Tazama:

> **Mwa 3:9,10** Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi? Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha.

Kwa kuwa Adamu alikumbatia uongo, aliamini kwamba ana uhai ndani yake. Shida ni kwamba sasa alitambua kwamba Mungu ni mkuu na ni chanzo cha uwezo wa maisha zaidi yake. Hii ilileta hofu. Wakati Adamu alikuwa hana imani kuhusu uhai ndani yake na alimuamini Mungu kwa furaha kwamba Mungu alikuwa Baba wa upendo ambaye alimpa kila kitu – hakuna hofu kama hiyo ingelikaribishwa. Tunda la kwanza la udanganyifu ni HOFU.

Jambo lingine ambalo udanganyifu ulileta ni kiburi. Wakati Adamu aliulizwa alichofanya, hangekubali kwamba alifanya makosa. Kiburi chake hakingemruhusu kufanya hivyo.

> **Mwa 3:11,12** Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo,nikala. .

Adamu alimlaumu mke wake. Angekumbuka kwa mfumo wa Mungu yeye ndiye kichwa cha nyumba yake; Majukumu yote kwa kweli yako juu yake kwa kile kinachoitendekea familia yake. Kumlaumu mke wake kulisaliti udanganyifu kwamba aliamini kwamba mke wake ana uwezo ndani yake wa kushinikiza tabia yake, na ndiyo maana angemlaumu na kutowajibika. Ni kweli Hawa alimjaribu Adamu, lakini alifanya uamuzi wake na kwa hivyo aliwajibika. Lakini hangekubali hivi. Tunda la pili la udanganyifu ni KIBURI.

Matunda haya mawili yalitengeneza mbegu za kuinuka kwa Babeli. Matunda ya uovu mengine zaidi ilibidi yaje. Adamu na Hawa walitubu makosa yao, lakini mbegu ya uasi ilikaa nao na ikapitishwa kwa wana wao Kaini na Habili.

Habili alipenda roho wa unyenyekevu wa Kristo na kwa unyenyekevu alifuata mpango wa Mungu aliouweka wa kuhifadhi kizazi cha binadamu ili kumkubali Mwana Wake tena. Kaini alimtambua Mungu lakini alikataa kufuata mipango yake. Hapa kuna tunda la tatu PINGAMIZI. Alibadili njia yake ya ibada ili imfurahishe na akapuuza kafara ya mwana kondoo. Habili alimsihi nduguye ili wafanye vile walivyoambiwa, lakini Kaini aliendelea kukataa na Shetani alimuongoza kumuua ndugu yake kikatili na hamaki. Hapa kuna matunda mengi zaidi: HASIRA, CHUKI NA MAUAJI. Mauaji ya Habili yalikuwa ni dhihirisho la mawazo ya Shetani dhidi ya Kristo. Habili mpole, mnyenyekevu alikatwa chini na nduguye ambaye alivuviwa na Shetani kama ushaidi wa kwanza wa hisia za kikatili zilizoelekezewa Kristo ambazo zilifichwa chini ndani ya moyo wa Shetani.

Kama tulivyosema hapo awali, roho wa upinzani anatowa kwetu hisia za baraka za Mungu na kibali. Bila baraka za Mungu tunajihisi kutokuwa na usalama. Kaini alikataa wazazi wake walivyomsihi, alikata ndugu yake alivyomsihi. Upinzani wa Kaini ulivyoongezeka, ndivyo kutokuwa na usalama na kutokuwa na thamani zaidi kulimfuata. Wakati Mungu alipotangaza laana juu ya kaini, hili lilikuwa si kitu ambacho Mungu alikuwa akimwekea, bali hili lilikuwa asili ya matokeo ya upinzani; hofu, kutokuwa na usalama na kutokuwa na thamani. Laana ilikuwa matokeo ya asili ya matendo ya Kaini – Mungu alikuwa akitaja.

> **Mwa 4:11,12** Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani.

Matamshi ya mtoro na mtu asiyekuwa na kikao yanapeana hisia za kutangatanga, kuyumbayumba na udhaifu. Haya ni matunda mengine: KUTOKUWA NA USALAMA, UDHAIFU NA KUTOKUWA NA THAMANI.

Wakati Adamu na Hawa walipompoteza Habili, Mungu aliwapa mwana mwingine – Sethi. Alidhihirisha wingi wa roho huyo wa unyenyekevu kama vile Adamu na Habili. Kwa hivyo makabila mawili ya chibuka katika familia ya Adamu; kabila la Sethi, ambalo lilijawa na hisia za baraka za Baba kwa unyenyekevu wa kutunza amri zake ambao walijulikana kama wana wa

Mungu na Kaini kutokuwa na thamani  walijulikana kama wana na binti za wanadamu.

Shetani alijua ya kuwa kwa sababu Mungu alifanya kiunzi cha uhusiano wa wanadamu katika familia, watoto walizaliwa ulimwenguni wakiwa wanawategemea wazazi wao. Hali hii ingewafunza watoto kumtegemea Mungu. Mtu muhimu kwa familia ambaye ilibidi awafundishe watoto kuhusu tabia muhimu ya unyenyekevu alikuwa mama. Shetani aliwajaribu wana wa Mungu kutafuta wana wa wanadamu ili kuwaoa. Binti za Kaini walijazwa na roho za baba zao: hofu, kiburi, upinzani, hasira na chuki. Matunda haya yote yalifichika katika moyo wa wanawake ambao walijifunza kutengeneza maumbile ya nje ya kupendeza. Wana wa Mungu hawakuweza kutambua tabia zao na wakawaoa wanawake hawa. Muungano huu ulisababisha watu wakatili wadhalimu. Bibilia inawaita mapandikizi ya watu, maana yake zaidi ya mapandikizi binafsi na inalenga kujilimbikizia mamlaka.

> **Mwa 6:1-5** Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao, wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua.  Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini. Nao Wanefili walikuwako duniani siku zile;tena ,baada ya hayo ,wana wa Mungu walipoingia kwa binti za binadamu,wakazaa nao wana;hao ndiyo waliokuwa watu hodari zamani ,watu wenye sifa. Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote.

Baada ya kipindi cha mda mchache, Roho nzuri ya Yesu ya unyenyekevu ilifutwa katika mioyo ya wana wa Mungu na mawazo ya karibu wote yalikuwa ni maovu kila saa. Mungu alitoa Roho Wake na akaruhusu gharika kuwekea uovu kikomo, uharibifu na ukatili. Aliwapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne. Mungu alianza tena na Nuhu na familia yake, lakini karibuni Shetani alipata mwanya kwa kupitia Hamu kwa kutengeneza misingi ya ufalme wa Babeli. Hamu alishinikizwa na watu waovu wa zamani. Siku moja alipompata babake katika hema yake uchi na amelewa, alimsumbua na kufanya naye kitu kibaya ambacho tunda la kutokuwa na thamani, udhaifu na upinzani lingesababisha kizazi chake kuweka mizani mipya ya urefu kwa utawala, uzuifu na uovu ilikutekeleza

kutokuwa na usalama na hofu iliyoongezeka. Nimrodi alikuwa ni mjukuu wa Hamu. Hivi ndivyo Bibilia inanena kumhusu:

> **Mwa 10:8-10** Kushi akamzaa Nimrodi, akaanza kuwa mtu hodari katika nchi. Alikuwa hodari kuwinda wanyama mbele za Bwana. Kwa hiyo watu hunena, Kama Nimrodi, hodari wakuwinda wanyama mbele za Bwana. Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari.

Neno hodari lina maanisha mdhalimu mwenye uwezo. Hakukuwa na kitu cha unyenyekevu kumhusu Nimrodi. Yeye ndiye mtu wa kwanza katika Bibilia kuchukua kichwa mfalme, na anaelezewa kwamba alijenga ufalme wake bila kumhusisha Mungu wa mbinguni. Mji wa kwanza wa ufalme wake ulikuwa Babeli au Babiloni. Sasa vile tumeweka msingi wa tabia ya Nimrodi, tunaweza sasa kuchunguza sehemu za dini aliyoianzisha.

Ukitaka kusoma zaidi mambo haya pakuwa kitabu Maisha ni muhimu kutoka kwa maranathamedia.com/kitabu/tazama/ maisha ni muhimu.

# 13 Kiini cha Babeli

Tukiangalia mambo yote ambayo yanafanya tabia ya Nimrodi, tunaweza kufikiria angelitengeneza mfumo gani wa ibada. Katika roho wa uasi, ingekuwa kinyume na kile Bibilia inafunua kumhusu Mungu na hiyo kwa haki ndiyo Nimrodi alitengeneza. Hapa mwana historia Josephus ananukuliwa akisema kile ambacho ni falsafa ya Nimrodi.

> "Sasa ilikuwa Nimrodi ambaye aliwasisimua kwa matusi na madharau kwa Mungu. Alikuwa mjukuu wa Hamu, mwana wa Nuhu, mtu mjasiri, na mwenye mkono wa nguvu. Aliwashawishi wasimtukuze Mungu kwayo (Nguvu), ati ni kwa sababu yake ndiyo maana walikuwa na furaha, bali ilikuwa kwa kupitia kwa ujasiri wa ambao ndiyo uliowaletea furaha. Alibadilisha ufalme ukawa ni wa udhalimu, akiona hakuna njia nyingine ya kuwafanya watu wasimche Mungu , bali kuwa weka kila mara wategemee nguvu zake..." Josephus kitabu cha kale 1, Sura 4, aya ya 2.

Nimrodi alikata katakata baraka za Mungu kwa kuchagua uwongo wa nyoka. Aliamua kuangazia uwezo baadala ya tabia. Aliwafundisha kujiangalia kama vile Shetani alivyo wafunza Adamu na Hawa. Hii filosofia ilikuwa na mgongano mkubwa katika muundo wa kifamilia. Hebu tazama vile mwana historia mmoja anavyosema:

> Mamlaka ya viongozi wa kitambo yalikuwa yamekita mizizi katika hisia za jamaa, na kupanda kwa mjumbe yalikuwa ni mfano wa kuongozwa na wazazi. Nimrodi, alikuwa ni kinyume, alikuwa ni enzi ya utawala, na watu ila tu walikuwa wakazi, bila kujali uhusiano wao, kwa hivyo kulikuwa na makabila - familia kubwa – jamii; sasa kulikuwa na nchi, jamii ya kisiasa – serikali. A.T Jones. Falme za Bibilia. 1904 Ukurasa 51

Mfumo wa mzee mkuu kuwa kiongozi ulisisitiza desturi ya baraka kwa kupitia utiifu kwa aliye kiongozi wa familia baba ikikuuzwa na mama. Nimrodi alibadilisha haya yote na akaangazia uongozi kwa kupitia mipaka na vitu vinavyoonekana kama mimea, mashamba, majumba. Familia ambazo zilikuwa zikifuga mifugo na kusonga na mifugo ziliongoza kwa kupitia hisia za kijamii. Msingi wa mamlaka yalikuwa heshima ya uhusiano. Nimrodi

aliamuru kwa kupitia hofu na kuwafanya watu wamtumikie kupitia udhalimu.

Nimrodi alichukua hatua nyingine ya kushangaza kwa kuvunja mfano wa Mungu katika uhusiano wa mume na mke. Nimrodi alimuoa mamake. Uhusiano wa tabia hii ya ndoa iko mbali sana ya kufikia uhusiano wa Baba na Mwana.

Wakati Nimrodi alipokufa, bibi yake/mamake Semiramis alisema ya kwamba Nimrodi aliingia kwa Jua na alikuwa mlinzi na mpaji wao. Semiramis alikuwa ndiye anayeunganisha maumbile na ulimwengu wa kiroho. Hivi ndivyo alivyopata kichwa "Malkia wa mbinguni" ( Yer 7:18) Kuungana naye ilikuwa ni njia ya kupata ulinzi na uwezo wa Nimrodi. Mfumo huu wa ibada ulinawiri na mfumo wa ibada ya Jua ikashika sehemu nyingi za dunia iliyokuwa ikijulikana. Siku ya jumapili ilikuwa ni siku kuu ya wiki ya ibada kinyume na baraka za kipekee za Mwana wa Mungu zinazokuja wakati wa masaa ya sabato. Mwa 2:3.

Semiramis alikuwa na mwana aliyeitwa Tamuzi. Ili kuhifadhi hali yake alisema kwamba alipata mimba kwa kupitia miyale ya Jua – Nimrodi. Nimrodi alikuwa amezaliwa tena katika Tamuzi. Hali ya kuzaliwa tena ililinganishwa na kuchipuka kwa mimea na ibada ya maumbile. Karamu ya kulilia Tamuzi ikaidhinishwa wakati wa msimu wa mimea kuwa kijani kibichi na msimu wa Jua ulipoisha. Ibada hii ilisimamiwa na sanamu ya (mama) Madonna aliyembeba mtoto.

> **Eze 8:14** Ndipo akanileta mpaka mlango wa kuingilia katika nyumba ya Bwana, ulioelekea upande wa kaskazini, na tazama, wanawake wameketi wakimlilia Tamuzi.

Kwa kupitia kwa Semiramis, mafundisho ya kuishi milele bila kufa yalianzishwa, kufanya mwanadamu kuwa mungu kwa jina la Nimrodi, ibada ya uwezo na mitindo mingi ya kuleta mvua na uzaaji vyote vilikuwa sehemu ya siri ya Babeli. Kwa kuwa Semiramis alikuwa ni njia yakufikia uwezo wa Nimrodi, kanuni ya dini ilianza ambapo mwanamume anaungana na mwanamke ili kupata nguvu. Hapo ndipo kulianza makahaba katika sehemu za ibada, na ibada ya Jua ilihusu ngono kama sehemu ya ibada. Hachukui nguvu nyingi kuona bila kuwajibika kifamilia, mfumo huu wa ibada ulionekana wa kuvutia kwa moyo wa kibinadamu.

Kidokezo muhimu ambacho tunahitaji kuelezea ni kwamba kama tamaa ya mamlaka ndiyo inakuwa lengo letu, utambulisho kamili kwa wale ambao tunatafuta kwao hauwi muhimu. Utambulisho wa mtu ni muhimu katika mfumo wa uhusiano ambapo uhusiano unatiliwa maanani. Mfumo wa ibada wa Babeli ulizunguka katika mambo ya watu watatu ambao uhusiano wao ulikuwa siri. Kwa sababu Nimrodi alikuwa mwana wa Semiramis, lakini tena bwana wake ambaye alizaliwa tena akiwa Tamuzi, utambulisho wa watu unakuwa giza. Kama vile tulivyosema, kujua utambulisho wa watu si wamaana kama uwezo au mamlaka ndiyo lengo lako la kuabudu. Hii ni kinyume kabisa na ibada ya Mungu wa mbinguni. Ni muhimu kujua utambulisho wa Baba na Mwana ili upate furaha na baraka za uhusiano wao. Utambulisho wa lazima usichanganywe, kuunganishwa au kufanywa siri. Wakati hali hii inatendeka tunaweza kuwa na uhakika kwamba ni mungu wa uwezo aliyeumbwa na Shetani ndiye anayeabudiwa, si Baba na Mwana wa Bibilia.

Katika uzoefu wangu na wa wale ambao nimehusiana nao katika Kikristo, nimepata mchanganyiko mkuu kuhusu yule ambaye anayezungumziwa katika mafungu mingine ya Bibilia na nani ambaye tunazungumza naye kwa maombi. Nimesikia watu wakidhihirisha machafuko wakati mwingi kuhusu yule kwa kweli wanayemuabudu, na bila kutaka kukasirisha kwa kumwacha mmoja nje. Machafuko haya yanatoka moja kwa moja kwa mfumo huu wa kibabeli na yanasaliti kutafuta uwezo baadala ya kumtafuta Baba na Mwana Wake na tabia zao. Hili linafanyika pasipo kujua kwa anayetafuta, kile kinachofundishwa ndicho kinachowaongoza kwa machafuko haya ya siri. Mfumo wa kibabeli ulianzishwa kuonyesha wanakiri kumuabudu, kumtukuza na kumpenda; bali kwa ukweli ni njia ya kumsahau na kumweka mwanadamu mahala Pake.

Ijapokuwa kuna mengi katika historia ya kutajwa kuhusu mfumo wa Babeli wa ibada ya Jua vidokezo muhimu ambavyo tunaangalia ni vya msingi wa falsafa kwa kulingana na kile Bibilia inafunua kuhusu Mungu. Mfumo wa ibada ya Nimrodi, Semiramis, Tamuzi inalenga yafuatayo:

1. Imani ya asili ya kutokufa.
2. Uwezo na nguvu kutoka ndani
3. Kukataa uongozi wa Baba/Mfumo wa baraka Kwa kukubali Mdhalimu - Uhusiano Mama na Mwana.

4. Uhusiano wa kifamilia uliodhohofika.
5. Wajenzi wa miji na kulenga kukusanya jimbo na mali.

Huu ndio utimilifu wa ahadi ya Shetani kwa mwanadamu kwamba mtakuwa kama miungu kwa kujua mema na mabaya. Mfumo wa ibada yoyote ambo una baadhi ya tabia hizi umeshinikizwa na ufalme wa Shetani. Hebu tukumbuke njia hii ya ibada imekuwa moja kwa moja kutokana na hofu, kiburi, uasi na mchafuko wa ngono ambao ni kinyume na Mungu aliyefunuliwa katika Bibilia.

## 14. Mstari wa Ukoo

Itakuwa jambo la kusaidia tukiangalia hatua zilizochukuliwa na Nimrodi na wenzake kwa kufanya mtazamo wao wa Mungu. Mtume Paulo anapeana maneno machache lakini ya dhahiri kuhusu wakati huu na vile ulivyoathiri wanadamu. Tutatumia haya kama kiunzi cha mjadala wetu.

Hapo mwanzo Mungu alimuumba mwanadamu kwa mfano Wake. Tuliona haya kwa Sura ya *Kuumbwa kwa Mfano Wake.* Mmoja ya sababu Mungu alimuumba binadamu vile alivyo fanya ilikuwa kufundisha ulimwengu zaidi kuhusu uhusiano Wake na wa Mwana Wake. Ona vile Paulo anasema:

> **Warumi 1:19,20** kwa maana yote yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao. Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani, uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru.

Ina maana kabisa kwamba Shetani angeshambulia uhusiano wa mume na mke ili kuzui hekima kuhusu Mungu kueleweka. Paulo anafuatilia historia ya Nimrodi kwa ufupi, tutafuatilia hatua kwa hatua.

> **Warumi 1:21-25** Kwa maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza Yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru, bali fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza. Ingawa wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga na kubadili utukufu wa Mungu aishiye milele kwa sanamu zilizofanywa zifanane na mwanadamu ambaye hufa, ndege, wanyama na viumbe vitambaavyo. Kwa hiyo, Mungu akawaacha wazifuate tamaa mbaya za mioyo yao katika uasherati, hata wakavunjiana heshima miili yao wao kwa wao. Kwa sababu waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe badala ya Mwumba, ahimidiwaye milele! Amen.

Kama vile mjuku wa Hamu, Nimrodi alikuwa kwa hakika anajua kuhusu Mungu wa mbinguni. Lakini wakati Nimrodi alikumbatia uongo kwamba nguvu hazikutoka kwa Mungu lakini ndani, alikoma kumtukuza Mungu au

kumpa shukrani kwa mibaraka ya Mungu. Hili lilimuongoza Nimrodi na wafuasi wake kwa uongo au hisia za ubatili kuhusu wao walikuwa kina nani? Majukumu ya wanaume kwa wanawake ambayo yalianzishwa na Mungu kwa makini yakageuzwa kabisa na kupotoshwa na ikakata mkondo wa baraka kutoka mbinguni. Roho nzuri wa unyenyekevu wa Mwana wa Mungu alizuiliwa kuingia katika nyumba zao na fikira zao zikawa na giza. Huo unaoitwa uhuru wa wanawake na uhuru mpya wa ngono ulioonekana kana kwamba ni maendeleo na busara, lakini iliwafanya wapumbavu.

Tuliona baada ya kifo cha Nimrodi, Semiramis alidai kuwa Nimrodi alikuwa Mungu akiwa ndani ya Jua. Dhana ya mungu ilikuwa inabadilishwa kuwa mwanadamu mfisadi. Mwanadamu alichafuka katika hisia zake kuhusu pahali uhai wake ulipotoka na muundo wa kiungu wa uhusiano wa mwanamume na mwanamke ulipotea. Uongo wa kumuabudu mwanamke ili kupata nguvu za Nimrodi, kuzaliwa kwa Nimrodi tena katika Tamuzi na ibada za kuabudu maumbile ambayo yalihusu kuabudu ndege, wanyama wenye miguu minne na wanaotambaa wote walitumika kuharibu mfano wa Mungu katika mwanadamu na kugeuza ukweli wa Mungu kuwa uongo.

Miungu ya Babeli ilikuwa kiini chake ibada ya kutafuta mamlaka. Kama vile tulivyosema hapo awali, utafutaji mamlaka unajali kidogo sana utambulisho wa viumbe vinavyoabudiwa, tabia yao haina maana kuliko mamlaka. Siri ya kuunganisha utambulisho wa nimrodi, Semiramis na Tamuzi na vile wanavyohusiana. Tendo la ngono lilikuwa muhimu zaidi kuliko utambulisho wa wale waliohusika, na ishara yake ikachukua maana tofauti.

> **Warumi 1:26-28** Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha wavunjiane heshima kwa kufuata tamaa zao za aibu. Hata wanawake wao wakabadili matumizi ya asili ya miili yao wakaitumia isivyokusudiwa. Vivyo hivyo wanaume pia wakiacha matumizi ya asili ya wanawake wakawakiana tamaa wao kwa wao. Wanaume wakafanyiana matendo ya aibu na wanaume wengine nao wakapata katika maisha yao adhabu iliyowastahili kwa ajili ya upotovu wao. Nao kwa kuwa walikataa kumkubali Mungu, Yeye akawaacha wafuate akili zao za upotovu, watende mambo yale yasiyostahili kutendwa.

Ushoga ni asili ya maendelo ya mfumo wa ibada ya Kibabeli. Tendo la ngono lilikuwa ndiyo njia ya kupata nguvu kwa yule aliyehusika, kama

ilivyoonyeshwa na mlinda lango Semiramis. Dhana ya uongozi na unyenyekevu haikuwa na maana. Mtazamo wa kibibilia kuhusu mume na mke unapotezwa kwa kutafuta ibada ya mtu binafsi na mamlaka. Paulo kisha anazungumzia matokeo ya mwisho:

> **Waru 1:29-32** Wakiwa wamejawa na udhalimu wa kila namna, uasherati, uovu, tamaa mbaya na hila. Wamejawa na husuda, uuaji, ugomvi, udanganyifu, hadaa na nia mbaya. Wao pia ni wasengenyaji, wasingiziaji, wanaomchukia Mungu, wajeuri, wenye kiburi na majivuno, wenye hila, wasiotii wazazi wao, wajinga, wasioamini, wasio na huruma na wakatili. Ingawa wanafahamu sheria ya haki ya Mungu kwamba watu wanaofanya mambo kama hayo wanastahili mauti, si kwamba wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia wanakubaliana na wale wanaoyatenda.

Watu wanashangaa kwa nini kuna ukatili mwingi, chuki na uasherati kwa wingi duniani! Warumi moja inatuonyesha wazi vile unavyofanya kazi. Kwa hivyo kwa muhtasari mstari wa kizazi ni kama ifuatavyo:

1. Kusahau kwamba uhai wote na baraka zinatoka kwa Baba na Mwana Wake.
2. Imani ya kwamba mtu ana asili ya chanzo cha uhai.
3. Kuharibu familia ambayo inahifadhi uongozi na mafundisho ya baraka kwa unyenyekevu.
4. Mchafuko wa ngono.
5. Kuongezeka kwa hisia za kutokuwa na thamani, hofu, kiburi ,hasira, chuki na mauaji kwa sababu ya kutokuwa na baraka.
6. Kumrudishia Mungu ufisadi wa uhusiano wa kibinadamu: Inamanisha kufanya utambulisho usionekane vizuri na kuabudu nguvu kuliko tabia.

Hii ndiyo hali ambayo ilishikwa na Babeli. Dhana ya Bibilia kuhusu Babeli ni zaidi sana kuliko ufalme wa kimaumbile. Inasimamia shambulio la kijeuri na la kikatili ambalo mwanadamu hajawahi fikiria. Na uwezo wake wa kuteka nyara akili wa shangaza. Hila ambayo inafanya nayo kazi ya stajabisha. Jinsi na njia ambayo inafanya kazi ni kwa namna nyingi. Nguvu za minyororo yake ni ngumu kuvunja iwapo umechukuliwa mateka ila- tu... Ila tu tujifunze hadithi ya Ibrahimu. Hadithi ya Ibrahimu inatupatia Kiini kilicho simuliwa cha kuokoka. Ni la muhimu ndiyo maana Paulo ananza barua yake kwa

Warumi kwa kuzungumzia Nguvu za Mungu kwa injili na kisha anatupatia kwa undani maisha ya Ibrahimu.

> **Warumi 1:16-18** Mimi siionei haya Injili ya Kristo kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwanza kwa Myahudi na kwa Myunani pia. Kwa maana katika Injili haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa, haki ile iliyo kwa njia ya imani hadi imani. Kama ilivyoandikwa: ''Mwenye haki ataishi kwa imani.'' Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu
>
> **Warumi 4:16-21** Kwa hiyo, ahadi huja kwa njia ya imani, ili ni kwa neema na itolewe kwa wazao wa Abrahamu, si kwa wale walio wa sheria peke yao bali pia kwa wale walio wa imani ya Abrahamu. Yeye ndiye baba yetu sisi sote. Kama ilivyoandikwa: ''Nimekufanya wewe kuwa baba wa mataifa mengi.'' Yeye ni baba yetu mbele za Mungu ambaye alimwamini, Mungu awapaye ahadi waliokufa na kuvitaja vile vitu ambavyo haviko kana kwamba vimekwisha kuwako.18 Akitarajia yasiyoweza kutarajiwa, Abrahamu akaamini atakuwa, ''Baba wa mataifa mengi,'' kama alivyoahidiwa kwamba, ''Uzao wako utakuwa mwingi mno.'' Abrahamu hakuwa dhaifu katika imani hata alipofikiri juu ya mwili wake, ambao ulikuwa kama uliokufa, kwani umri wake ulikuwa unakaribia miaka mia moja, au alipofikiiri juu ya ufu wa tumbo la Sara. Lakini Abrahamu hakusitasita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu, bali alitiwa nguvu katika imani yake na kumpa Mungu utukufu, akiwa na hakika kabisa kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kutimiza lile aliloahidi.

Hadithi ya Ibrahimu kutoroka Babeli ni moyo wa injili wa Kristo; ndiyo hadithi ambayo tunayoigeukia kufuata ili tujifunze njia ya kuepuka hatua hizi 6 za mstari wa uzao, na kuvunja minyororo ya Babeli na kilio “umeanguka Babeli”

## 15. Wito wa Kutoka Babeli

Ibada ya sanamu ya siri ya Babeli ikaenea ulimwenguni. Bibilia inasema:

> **Yer 51:7** Babeli umekuwa kikombe cha dhahabu mkononi mwa Bwana; kilicholevya dunia yote; mataifa wamekunywa mvinyo wake; kwa sababu hiyo mataifa wameingiwa na wazimu.

Mvinyo wa Babeli ni mafundisho yake ya siri kuhusu Mungu ambayo yanachanganya akili kama imelewa. Mafundisho haya yanaharibu familia, na kukatisha baraka za Baba wa mbinguni, na inaleta hisia za ndani za kutokuwa na thamani, hasira, kutokuwa na usalama ikiongezwa na tamaa ya nguvu.

Ushawishi wa Babeli uligeuza hali ya familia ya kuzunguka na mifugo katika makabila hadi kuwa na utawala uliokuwa na majeshi. Vijiji vidogo viligeuka kuwa miji mikubwa iliyozungukwa na kuta kwa ulinzi rahisi. Njia ya kutoza ushuru ilibidi itengenezwe ili kuwapatia majeshi chakula na silaha. Utoza ushuru ilibidi kuwe na utawala wa udhalimu ili kuhakikisha ushuru ulikusanywa. Kuangalia kila mara damu iliyomwagika kulifanya watu wawe na mioyo migumu na pia kuongezeka kwa saa mbali na familia ikiongezwa na matendo ya uasherati ya ibada ulifanya ukahaba kuongezeka, ambao ulivunja familia na kuwatendea wanawake vizuri kidogo kushinda ng'ombe, ila tu wawe makahaba wa hekalu ambao walitunzwa vizuri.

Njia hii ilikuwa ni mipango yote ya Shetani kuharibu mfano wa Mungu, kumvua heshima na kumfanya mtumwa wa malengo yake kwa vita vyake dhidi ya Mungu. Mungu alijibu kwa upendo wa huruma na kumuita mtu kuengeneza ufalme wa familia ambao msingi wake ulikuwa ni majukumu ya baba kubariki na pia kurudisha tabia muhimu - na kukuuza mke mnyenyekevu wa kufunza kizazi cha baadaye kunyenyekea kwa Mungu wa mbinguni na Mwana Wake. Ibrahimu au Abramu kama alivyoitwa hapo awali, aliishi kidogo tu baada ya wakati wa Nimrodi ijapokuwa wengine wanashauri maisha yao yalipishana, wakati dini ya kibabeli ilishika dunia yote.

> **Mwa 12:1-3** Bwana akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi

> nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa.

Mahali ambapo Abramu alistahili kuishi kulikuwa ni moyo wa ufalme wa Nimrodi, Kaldayo.

> **Mwa 11:26-28** Tera akaishi miaka sabini, akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani. Na hivi ndivyo vizazi vya Tera. Tera akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani. Harani akamzaa Lutu. Harani akafa kabla ya baba yake Tera katika nchi aliyozaliwa, yaani, katika Uru wa Wakaldayo.

Mungu alimtoa Abramu mbali na mahali alilelewa utotoni ili kuvunja uhusiano na marafiki zake na mitindo ya ibada aliyokuwa na uzoefu nayo. Mungu angembariki Abramu na elimu ya ufalme wa familia ambao msingi wake ni uhusiano wa Baba na Mwana. Mungu alizuia uwezo wa Sara wa kuza mpaka wangejifunza kabisa mambo haya ya busara.

Mungu alifanya baraka kwa kuanzisha utaratibu vile familia inastahili kuwa. Wote ambao walimuiga Sara katika mambo ya busara kuhusu familia wangepata ufunguo wakupokea baraka za Baba wa mbinguni ndani ya mioyo yao na kuwapatia hisia za nguvu kwamba wanapendwa vile walivyo na si kwa nguvu walizonazo. Ahadi ya ufalme mkuu kwa Abramu ulikuwa na masharti kwa muundo wa familia uliowazi.

> **Mwa 18:18,19** akiwa Ibrahimu atakuwa taifa kuu, hodari, na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa? Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana, wafanye haki na hukumu, ili kwamba Bwana naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake.

Fungu la maneno “Kwa maana nimemjua” linatupatia hisia za uhusiano wakaribu sana kati ya Mungu na Ibrahimu kwa kuwa Mungu alimfunza jinsi ya kutunza mke wake na watoto. Alimuelezea kwamba ilibuniwa tangu awali kwamba bwana na Baba wawemkondo wakupokea baraka kutoka kwa Baba wa mbinguni kwa kufurahishwa nao. Si pekee tu bwana na baba walikuwa

na mbegu ya kimaumbile kukuzwa na mkewe kuwa watoto, lakini pia alistahili kupeana mbegu ya kiroho kumpa bibi yake hisia za kukubalika na upendo na watoto lengo na thamani. Tazama vile mithali inavyosema.

> **Mit 17:6** Wana wa wana ndio taji ya wazee, Na utukufu wa watoto ni baba zao.

Uwezo wa Ibrahimu kumbariki mke wake na watoto wake ulitegemea sana roho ya unyenyekevu ya Sara; mamlaka yake yalikuwa makubwa kadiri alivyopewa na yeye. Vile alizidi kuombea uongozi wake na kuamini maneno ya bwana wake, ni zaidi watoto wake wangeliona kile alichosema ni cha maana. Watoto wanaangalia mama yao kujua umuhimu na uzito wa neno la baba yao. Mtume Petero anatuambia vile Sara alijivunza kumuangalia mume wake.

> **1 Petero3:5,6** Kwa kuwa hivi ndivyo walivyokuwa wakijipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu. Wao walikuwa ni watiifu kwa waume zao, kama Sara alivyomtii mumewe Abrahamu, akamwita 'bwana.' Ninyi ni watoto wa Sara kama mkitenda yaliyo mema na bila kuogopa jambo lo lote.

Kwa kuwa Ibrahimu na Sara walitoka Babeli walikuwa na mengi ya kujifunza. Wote walifanya makosa ambayo yalichelewesha kuzaliwa kwa Isaka na Sara. Baada ya majaribu mengi, Ibrahimu na Sara walimruhusu Mungu ambariki Isaka na Roho ya Mwana wake mpaka Isaka alikubali kunyenyekea hadi kifo kama vile Kristo alikubali kufa msalabani. Ibrahimu pia alijifunza kuthamini roho ya unyenyekevu kwa kuamua kumuamini Mungu hata kama ilikuwa haiwezekani.

> **Mwa 22:1,2,10-12** Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe. Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana

> sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee.

Ni jambo la kushangaza kufikiria kwamba katika maisha ya mtu mmoja, Mungu aliweza kuvunja utumwa wa mfumo wa siri ya Kibabeli katika fikira zake na kurudisha ibada ya Mungu wa kweli wa mbinguni. Safari ya Ibrahimu kutoka Babeli ni msingi muhimu kwa safari yetu leo. Mungu wa kweli wa mbinguni na Mwana Wake anatuita kutoka kwa miungu ya uongo ya dunia hii na tuingie katika uhusiano wa ufalme wao pahali ambapo thamani inatokana na uhusiano wa kifamilia na si kwa vitu tunavyofanikisha.

Mafunzo ya busara katika kijitabu hiki yamefafanuliwa katika kitabu Maisha ni ya Maana. Katika mtandao maranathamedia.com. Tafadhali pata nakala ya kitabu hiki kwa maelezo zaidi kuhusu mfumo wa baraka ya familia ambayo inashinda ufalme wa Shetani kwa kupitia elimu ya kweli kumhusu Mungu na Mwana Wake.

# Hekima ya Mungu

Yeye aliye na Mwana anaouzima. Mbona hili liko hivyo? Kwa maana katika Mwana wa Mungu panaishi moyo mtakatifu wa Mwana mtiifu kwa Baba yake. Daima anafanya mambo ambayo yanampendeza Baba. Pia anayomibaraka na upendo wa kina wa Baba. Moyo wa Mwana unapumzika kikamilifu katika upendo wa Baba yake.

Ni hekima ya Baba kugawa Roho wa Mwanawe mpendwa kwa ulimwengu; Roho tamu, wa upole na mtiifu ambaye anapenda amri za babake. Kristo ni hekima ya Mungu na usalama wa kupenda ufalme wa mahusiano.

Roho huyu mpole anatiririka kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu kupitia kwa mti wa uzima. Shetani alimkataa Mwana wa Mungu na Roho wake wa upole. Roho wake wa uasi alikuwa vitani na Roho mpole, mnyenyekevu na mtiifu wa Mwana wa Mungu. Roho huyu wa uasi alipitishwa kwa jamii ya mwanadamu. Katika kafara ya Kristo tunapewa tena Roho huyu mpole. Siri ya kuwa na Roho huyu ni kujua Baba na Mwana ni akina nani – huu ni uzima wa milele kumjua Baba na Mwanawe na kunywa kutoka kwa chemchemi ya maji ya uzima yanayobubujika kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu na Mwana kondoo.